

**JAMUHUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA NACHINGWEA**

SHULE YA SEKONDARI KILIMARONDO,
S.L.P 49,
NACHINGWEA,
LINDI,
TAREHE.....

KUMB. NA. K'RONDO SS

NDUGU MZAZI/MLEZI WA.....

**YAH; MWANAO KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA ELIMU YA SEKONDARI
KIDATO CHA KWANZA KILIMARONDO SEKONDARI MWAKA 2021.**

Nafurahi kukujulisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari kidato cha kwanza katika shule ya sekondari kilimarondo hongera sana.

Muhula wa kwanza utaanza tarehe 11/01/2021 hivyo basi mwanafunzi anatakiwa kuripoti tarehe 11/01/2021 akiwa na mzazi/mlezi wake. Masomo ya msingi atakayojifunza ni uraia, historia, jiografia, Kiswahili, lugha ya kiingereza, kemia, Fizikia, biologia, na hisabati. Masomo ya mchepuo kama vile biashala na kilimo yatategemea na upatikanaji wa walimu.

shule ipo katika kata ya kilimarondo umbali wa kilomita mbili na nusu upande wa magharibi kutoka makao makuu ya tarafa.

Aidha shule hii ni ya kutwa na ni mchanganyiko wa wavulana na wasichana.

Nakutakia maandalizi mema.

Ahsante.

.....
NKWAYA J. KUBILU

MKUU WA SHULE.

MAHITAJI YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KILIMARONDO

A. SARE ZA SHULE

I. WASICHANA

- a. Siketi mbili ndefu za rangi nyekundu damu ya mzee.
- b. Shati mbili nyeupe aina ya tetroni za mikono mifupi.
- c. Viatu vya ngozi rangi nyeusi jozi mbili vyenye visigino vifupi.
- d. Soksi ndefu za rangi nyeupe tupu bila kuchanganyikana rangi nyingine.
- e. t-shirt za shule mzazi/mlezi achangie tsh 15000/=
- f. kwa watoto wakike wa kiislamu kama atavaa hijabu azingatie yafuatayo;
 - ✓ nusu kanzu inayofika magotini .
 - ✓ sketi iwe ndefu
 - ✓ hijabu iwe ndefu ifike magotini
- g. Aje na ream moja A₄

II. WAVULANA

- a. surualimbili za rangi nyekundu damu ya mzee zenyenye rinda namifuko mitatu [nyuma mmoja na mbele miwili]
- b. Shati mbili nyeupe aina ya tetroni za mikono mifupi.
- c. Viatu vya ngozi rangi nyeusi jozi mbili vyenye visigino vifupi(visiwe buti)
- d. Soksi ndefu za rangi nyeupe tupu bila kuchanganyikana rangi nyingine.
- e. Mikanda miwili ya ngozi ya rangi nyeusi bila ya kuchanganya na rangi nyingine.
- f. T-shirt za shule mzazi/mlezi achangie tsh 15000/=
- g. Ae na ream moja A₄.

Hatutampokea mwanao hapa shulenii endapo wewe mzazi/mlezi utanunua sare tofauti na maelekezo ya shule.

B. MAVAZI YA KAZI ZA NJE YA DARASA NA MICHEZO

- a. **t-shirt** yenye nembo ya shule
- b. viatu vya michezo mfano raba n.k (michezo ni lazima kwa wote)
- c. bukta ya rangi ya bluu kwa wote au traksuti ya bluu kwa wote

C. MICHANGO YA SHULE

michango ya shule ni kama ifuatavyo;

- a. Mahindi **kg 30** kwa mwaka
- b. Fedha kwa ajili ya mpishi **Tsh 30,000/=**
- c. Mboga jamii ya kunde/mbaazi **kg 15** kwa mwaka

D. MAHITAJI YA DARASANI

- a. Daftari kubwa [10] aina ya [counter quire three [3]
- b. mkebe [Mathematical set] Rula,pencel,peni [kalamu ya winozakutosha.
- c. Begi la mgongoni [Hatuhitaji mifuko ya Rambo.
- d. Dictionary English to Kiswahili [oxford].

E. VIFAA VYA USAFI NA KAZI ZA NJE

- a. Fagio za chelewa mbili.
- b. Ndoo ndogo ya plastiki moja.
- c. Chagua fungu moja kati ya yafuatayo.
 - panga moja jipya
 - kwanja moja jipya
 - jembe moja jipya lenye mpini
- ❖ Hatutapokea vifaa vya mtumba [vilivyo tumika]
Tafadhal soma kwa makini maelekezo na maagizo na uyekeleze kikamilifu.
Tunakutakia maandalizi mema na karibu sana Kilimarondo sekondari.

✓ AJE NA CHETI CHA KUZALIWA[COPY]

- ❖ **MHUMIMU;** Fomu ambayo imeambatanishwa katika barua hii kwaajili ya kupima Afya anatakiwa akapimwe kituo cha Afya Kilimarondo au Hospitari ya wilaya Nachingwea na sio zahanati.
 - ✓ Kama mwanao anatatizo la kudumu la kiafya lililozibitika aje na cheti cha tatizo husika kilichodhibitika na daktari.

.....

NKWAYA J. KUBILU

MKUU WA SHULE

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

1. Mwanafunzi anawajibika kuwa na heshima na adabu kuanzia nyumbani, shulenii na mitaani.
2. Mwanafunzi hatakiwi kutoroka vipindi vya masomo, kutumia lugha mbaya, matusi kati yake na wanafunzi wenzake na watu wote.
3. Kuhestimu wimbo na Bendera ya Taifa na nembo za Taifa kama kusimamia wima (kikakamavu) wakati wa kuimba, kupandisha na kushusha Bendera ya Taifa
4. Ni lazima mwanafunzi awe mwadilifu, mwaminifu na mkweli wakati wote
5. Mwanafunzi anatakiwa kusimama na kupokea mzigo wa mwalimu au mfanyakazi asiye mwalimu.

Mwanafunzi haruhusiwi kufanya mambo yafuatayo:-

- (i) Kuvuta sigara / bangi au kutumia madawa ya kulevyaa
- (ii) Kuvali mavazi na mitindo isiyo ya heshima, mfano mlegezo, sketi fupi n.k
- (iii) Kupiga kelele darasani au mabwenini wakati wa usiku na mara baada ya kutoka kujisomea (Night preparation)
- (iv) Kunyoa mitindo isiyokubalika kama vile, pank, kipara, kiduku au kunyoa nywele ambazo haziwezi kushikika (ndogo sana)
- (v) Kufuga nywele mpaka kuwa ndefu sana, kuacha kucha ndefu na kufuga ndevu
- (vi) Utoro wa kudumu au utoro wa vipindi (utoro wa rejareja) unatakiwa kuhudhuria vipindi vyote bila kukosa
- (vii) Kuonekana anapika au kuingia jiko la shule bila sababu maalum, haruhusiwi kuingia kama si kiongozi wa zamuu
- (viii) Kuongeza mapambo au urembo nje ya sare za shule kama vile bangili, mkufu, ereni, pete, kacha (shanga za shingoni au mgononi) kujipaka rangi za kcuha au mdomoni, kuweka dawa za nywele (kali) hasa wasichana.
- (ix) Kuonekana katika maeneo yafuatayo:- Vilabu vya pombe (baa), nyumba za kulala wageni (Guest House) bila sababu maalumu, kumbi za starehe isipokuwa akiwa na mzazi/mlezi.
- (x) Kumiliki au kutumia simu shulenii, kuandika maandishi ukutani au sakafuni

Makosa yafuatayo yataapelekea mwanafunzi afukuzwe shule.

1. Kutumia madawa ya kulevyaa
2. Uasherati, kupata/kusababisha mimba
3. Wizi
4. Kushiriki vitendo vya kishirikina
5. Kukosa kwa makusudi kufanya mitihani
6. Kugomea adhabu
7. Kupiga/kupigana
8. Kudharau bendera na wimbo wa taifa, fedha za taifa na picha za viongozi
9. Utoro wa kuanzia siku (90) tisini
10. Kuharibu kwa makusudi mali ya serikali
11. Kuanzisha au kushiriki mgomo

AHADI YA KUKUBALI KUJIUNGA NA KUKUBALI SHERIA ZA SHULE

Mimi mwanafunzi niliyechaguliwa
kujiunga katika shule hii (Matekwe Sekondari) mwaka 2021.

1. Nakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga kidato cha kwanza mwaka 2021
2. Naahidi kwamba nitatii sheria zote za shule niliyotumiwa kabla ya kujiunga na shule
3. Nitafuata masharti na maagizo yote nitakayopewa na walimu au viongozi mbalimbali wa shule.

NATOA AHADI YANGU MBELE YA MZAZI/MLEZI WANGU

Bwana / Bibi/ Ndugu

Saini yake

.....
SAHIHI YA MZAZI/MLEZI

TAREHE

NAMBA YA SIMU YA MZAZI/MLEZI

.....
SAHIHI YA MWANAFUNZI

TAREHE

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF EDUCATION AND VOCATIONAL TRAINING**

KILIMARONDO SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 49,
NACHINGWEA.

REF NO.

DATE

TO. The Medical Officer

.....
.....

REF. (Name in full)

Please examine the above named student.

The examination should include the following category (a-d)

- a) (i) Eyesight (ii) Hearing (iii) Speech (iv) Limbs (v) Venereal diseases (vi) Leprosy
(vii) Epilepsy
- b) Neurosis
- c) Other serious disease e.g Asthma, Tb Etc.

PART B: MEDICAL EXAMINATION

(To be completed by a Government Medical Officer). I have examined the above named student and consider that she is **FIT/UNFIT** for full time students.

- (i) Eyesight
- (ii) Hearing.....
- (iii) Speech.....
- (iv) Limbs.....
- (v) Venereal diseases.....
- (vi) Leprosy.....
- (vii) Epilepsy.....
- (viii) Neurosis.....
- (ix) Other serious diseases eg. Asthma.....
- (x) T.B.....
- (xi) Pregnancy

Other comment

.....
.....

Name **Date** **Signature**

STATION **DESIGNATION**